**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,**
Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa utukufu, kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, nikushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Baraza hili tukufu. Ni imani yetu kwamba utaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha Demokrasia katika chombo hichi muhimu cha wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kazi nzuri na kubwa ya kutuletea maendeleo nchini. Vile vile, tunawapongeza wasaidizi wake Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Othman Masoud Othman na Mhe. Makamu wa Pili Hemed Suleiman Abdulla kwa kumsaidia vyema Mhe. Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,**
Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu kwani kuchaguliwa kwetu kuja kuwawakilisha wananchi, ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi ahadi yetu kwao ni kwamba tutawatumikia kwa dhati kama ambavyo walivyotuamini kutuleta katika chombo hichi kwa lengo la kutetea maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika,**
Sina budi pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia Makadirio ya

Bajeti ya Wizara hii. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi ya kuongoza kikao kuwa nyepesi na ya ufanisi.

Kwa kweli, ni wajumbe Mahiri, ambao wameweza kuyajadili kwa kina na ipasavyo makadirio hayo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha zinatumiwa kwa matumizi yaliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa heshima ya hali ya juu napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mheshimiwa Mohammed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| *2.* | Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mheshimiwa Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *4.* | Mheshimiwa Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| *5.* | Mheshimiwa Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| *6.* | Mheshimiwa Zawadi Amur Nassor | Mjumbe |

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi na makatibu wawili (2) pamoja na msaidizi wa Mjumbe mmoja (1) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu, makatibu hao na msaidizi ni:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Ndugu Fatma Omar Ali | Katibu |
| *2.* | Ndugu Mussa Issa Mussa | Katibu |
| *3.* | Ndugu Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**
Ikumbukwe kwamba miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa katika Kanuni ya 107(3)(v) Kamati yangu ilikaa na kuijadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati nawasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya utangulizi huo sasa naomba nitekeleze jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako tukufu moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,**
Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha **2023/2024** ina fungu (vote) **moja (1)** ambalo ni **J03** na imepanga kutekeleza **Programu Kuu Nne (4) zenye Programu Ndogo Nane (8)** ambapo kwa ujumla fedha zilizoombwa kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ni **TZS. 51,939,984,000 (Bilioni Hamsini na Moja, Milioni Mia Tisa na Thelathini na Tisa, Laki Tisa na Thamanini na Nne).**

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

**Mheshimiwa Spika,**
**Programu Kuu** hii inatekelezwa chini ya **Programu Ndogo** mbili ambazo ni **SJ030101 Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na SJ030102 Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji,** ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 **Programu Kuu** hii imepangiwa jumla ya **Shilingi 8,069,311,000/= (Bilioni Nane, Milioni Sitini na Tisa, Lakii Tatu na Elfu Kumi na Moja),** ambapo mwaka fedha 2022/2023 ilipangiwa jumla ya **Shilingi 22,980,061,000/= (Bilioni Ishirini na Mbili, Milioni Mia Tisa na Thamanini na Elfu Sitini na Moja).**

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inasikitishwa kuona bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni ndogo ukilinganisha na bajeti iliyopita. Kutokana na hali hiyo, Kamati inawasiwasi utekezaji wa majukumu yaliyopangwa kushindwa kutekelezeka kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa.

## PROGRAMU NDOGO YA UPATIKANAJI NA USAMBAZAJI WA HABARI

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati haikuridhishwa kuona Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) kusitishiwa kuingiziwa fedha za Ruzuku kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kila siku. Kamati, baada ya kubaini suala hilo wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ilimuomba Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kukaa na watendaji wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa lengo la kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala hilo, licha ya kwamba Serikali ilikuwa na lengo la kulitaka Shirika hilo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 lisitengewe fedha

yoyote kwa ajili ya Ruzuku ili lianze kujitegemea kama yalivyo mashirika mengine duniani.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati, ilipinga suala hili la *ZBC* kutotengewa fedha yoyote ya Ruzuku kwa mwaka huu, kwani kiuhalisia Shirika hilo bado ni changa na linahitaji kuendelezwa ili liweze kujitegemea wenyewe na kuchangia mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na mjadala mkubwa uliofanyika, Kamati inaishukuru Serikali kwa kukubaliana na mapendekezo ya Kamati ya kuitengea fedha za Ruzuku Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya **Tsh. 4,937,500,000/= (Bilioni Nne, Milioni Mia Tisa na Thalathini na Saba na Laki Tano)**, kwani huduma hii ilikuwa haikutengewa fedha yoyote ya utekelezaji kwa mwaka huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia, Kamati inalishauri Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) kukuza na kuvisimamia vyanzo vyao vya mapato ya ndani na kutafuta vyanzo vyengine vipya kwa ajili ya Shirika kuweza kusimama wenyewe bila kutegema fedha ya Ruzuku kutoka Serikalini ili liweze kuendana na azma ya Serikali ya Awamu ya Nane kwamba Mashirika yote yaweze kujiendesha wenyewe.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inashangazwa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kushindwa kutoa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo iliyopitishwa na Baraza lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kuhusu Ununuzi wa Vifaa na Mitambo ya ZBC jumla ya **Tsh. 12,337,261,000/= (Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Tatu na Thalathini na Saba, Laki Mbili na Sitini na Moja Elfu)**, ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 miradi hiyo haikupangiwa fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wake licha ya mchakato wake wa manunuzi ulikuwa umeshakamilika kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA VYOMBO VYA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa **Programu Ndogo** ya SJ030102. Kamati, haikufurahishwa kuona huduma hii ya **HJ03010202** kwa mwaka wa

fedha 2022/2023 fedha zilizoidhinishwa na Baraza kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa hazikupatikana.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kutenga fedha kwa ajili ya Wakala wa Uchapaji wa Serikali (*ZGP*) kwa ajili ya kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na hatimaye kuweza kujiendesha wenyewe na Serikali kupata gawio kutoka kwa Wakala kwani hilo ndilo lengo kuu la kuanzishwa kwake.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upande wa fedha za miradi ya Maendeleo Kamati inashangazwa kuona kwa mwaka huu wa bajeti 2023/2024 fedha za ununuzi wa mitambo ya kisasa hazitengwa na za mwaka uliopita zilizopitishwa na Baraza lako tukufu jumla ya **Tsh. 2,000,000,000/= (Bilioni Mbili)** hadi kufikia mwezi wa Machi 2023 hazijapatikana. Kutokana na hali, imepelekea Wakala kukosa baadhi ya kazi na kubakia kufanya kazi katika mazingira magumu, kwani mitambo iliyopo inafanya kazi kuliko uwezo wake, hivyo huharibika mara kwa mara na kupelekea Serikali kuikosesha mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa na Wakala huo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA

**Mheshimiwa Spika,**
Programu hii ya PJ0302 inatekelezwa kupitia huduma mbili kuu ikiwemo ya Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Maendeleo ya Vijana pamoja na Kusimamia Uendeshaji wa Mabaraza ya Vijana.

**Mheshimiwa Spika,**
Kama inavyofahamika kuwa lengo kuu la kuanzishwa kwa Programu Kuu hii ni kuwasaidia na kuwaendeleza vijana wasiokuwa na uwezo wa kuajiriwa na Serikali nao kuweza kujikimu, kujitegemea na kujiendesha kimaisha kama walivyo watu wengine.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 programu hii ilitengewa jumla ya **Tsh. 6,400,000,000/= (Bilioni Sita na Milioni Mia Nne)** kwa ajili ya kuratibu na kusimamia shughuli za Maendeleo ya Vijana cha kushangaza fedha iliyopatikana hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya **Tsh. Milioni 353,035,385/= (Milioni Mia Tatu na Hamsini na Tatu, Thalathini na**

**Tano Elfu na Mia Tatu na Thamanini na Tano)** ni kidogo isiyoweza kufanikisha malengo yaliyopangwa kwa mwaka husika.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na hali hiyo, Kamati haijaridhishwa na hatua ya Serikali ya kutotenga fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za vijana kwani ni kwenda kinyume na azma na malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025 na maono ya Mhe. Rais wetu mpendwa wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa vijana.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,**
Katika **Programu Kuu** hii, Kamati itajikita zaidi katika **Programu Ndogo ya SJ030302** ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya pamoja na Mikoa yote kwa Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yangu inapenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa juhudi kubwa wanazochukua za kuleta maendeleo katika Sekta ya Michezo Zanzibar ikiwemo uimarishaji pamoja na ujenzi wa viwanja mbali mbali vya michezo kwa Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yangu inaendelea kuishauri tena Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuandaa utaratibu madhubuti juu ya usimamizi na ufuatiliaji wa Miradi hiyo, ili yasije kujitokeza mapungufu kama yalionekana katika Miradi iliyopita ya ujenzi wa Viwanja wa Wilaya Unguja na Pemba. Mfano halisi wa hayo, Kiwanja cha Kangani, Kiwanja cha Kishindeni, Kiwanja cha Kitogani, Kiwanja cha Mkokotoni pamoja na Kiwanja cha Kama.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, Kamati inashauri Serikali kuwatilia fedha Wakandarasi na Mshauri Elekezi wanaoufanyia matengenezo uwanja wa Michezo wa Gombani ili kuepusha kuongezeka muda wa kazi kwa Mkandarasi, hivyo kuongeza gharama za matengenezo.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwisho, napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, kwa vile Kamati yangu ya Ustawi wa Jamii imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2023/2023, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha ujao.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba ya Mwenyekiti wangu pamoja na Kamati ya Ustawi wa Jamii, naunga mkono hoja.

**Mheshimiwa Spika,**
Naomba kuwasilisha.

……………………..,
**Mohammed Ahmada Salum,**
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**